JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

***Dar es Salaam, 20 Oktoba, 2025***

# TAARIFA KWA UMMA

## KUKAMILIKA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inaufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na wadau wa Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kuwa udahili katika Awamu ya Tatu na ya mwisho kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2025/2026 umekamilika. Majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Tatu yanatangazwa na vyuo husika.

### 2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale ambao hawakuweza kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita, **wanapaswa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia tarehe 20 Oktoba hadi 03 Novemba, 2025.** Uthibitisho huo unafanyika kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba namba hiyo ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Aidha, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Kwa urahisi wa rejea, orodha ya majina ya waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja inapatikana kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

## 3.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa
**KATIBU MTENDAJI**
**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz